SWALI: Naomba kufahamu nini maana ya huu mstari,

> *Mithali 16:2 “Njia zote za mtu ni safi machoni pake mwenyewe; Bali Bwana huzipima roho za watu”.*

---

JIBU: Kama vile Biblia inavyosema moyo huwa mdanganyifu kuliko kitu kingine chochote, (Yeremia 17:9), ikiwa na maana ni kawaida ya mwanadamu, kuziona njia zake zote alizozichagua ni sawa mbele zake, ni mara chache sana, kusikia mtu anakiri kuwa uamuzi anaoufanya ni wa kishetani,

Nimekutana na waganga wa kienyeji wanasema kitu tunachokifanya ni sawa, hakina madhara yoyote, ukienda kwa waabudu sanamu, watakuambia vivyo hivyo hizi ni ishara tu, tunaabudu Mungu yuleyule, Ukienda kwa wauza pombe watakuambia nao maneno hayo hayo  n.k… Kwasababu biblia inasema njia “ZOTE” (sio moja) za mtu ni safi machoni pake mwenyewe.

Lakini Bwana huzipima roho za watu. Ikiwa na maana, Mungu

anazichunguza nia zetu. Yeye hashawishwi na kile tunachokiona ni sawa, kwa macho yetu, au kwa mitazamo yetu, bali anatazama ndani Zaidi ya mwanadamu, anaweka kwenye mizani, anatazama nia, ya mtu ilikuwa  ni nini, na matokeo yake yatakuwa ni nini mwishoni..

Kwamfano Mafarisayo na Masadukayo, walijihesabia haki, kwa mapokeo yao, wakijiona kuwa ni watakatifu, na bora kuliko wengine, lakini Bwana Yesu aliwaita wanafki. Kwasababu, kazi yao ilikuwa ni kusafisha kikombe kwa nje tu, lakini ndani ni kuchafu, wanafunga ili waonekane na watu, wanaomba ili waonekane ni wazuri katika mambo hayo. Walikuwa wanajifanya kumwita Yesu Rabi, lakini ndani wamejaa wivu. (Mathayo 23:1-39)

Hivyo nasi twapasa tulijue hilo, ili tusidanganyike.

Kitabu cha 1Wakorintho 13, inasema nijaposema kwa lugha za wanadamu na Malaika, nijapoutoa mwili wangu uungue moto, nijapotoa mali zangu zote niwape maskini, nijapokuwa na unabii, na Imani timilifu ya kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo mimi si kitu, ni sawa na bure tu.

Waweza kuwa mhubiri mzuri, mkubwa, unaokoa roho za watu,

nawe ukaona njia hiyo ndiyo inayompendeza Mungu zaidi, lakini ndani yako unahubiri kwasababu ya fitina, kama inavyosema Wafilipi 1:15, au upate umaarufu, au upate fedha,.ujue unachokifanya ni bure.

Hivyo, katika lolote tulifanyalo, ili liwe na faida njema nyuma yake, lazima tujue nia yetu ya dhati kufanya hivyo ni nini, Ndicho Bwana anachokitazama sana, kuliko, hichi cha nje tukionyeshacho.

Kulikuwapo na wale watu, waliokataa, kwenda harusini walipoalikwa, na ukitazama kibinadamu sababu za wao kutokwenda zina mashiko kabisa, mwingine anasema ninaoa, hivyo ni sharti niwe na mke wangu kwa kipindi hiki, lakini Bwana Yesu aliona kama ni UDHURU wanatoa wote, kwasababu yeye ndio anayechunguza mioyo, akaona kutoa kwao udhuru ni kwasababu hawakuthamini wito wake tangu mwanzo.

> *Luka 14:16 “Akamwambia, Mtu mmoja alifanya karamu kubwa akaalika watu wengi,*
>
> *17 akamtuma mtumwa wake saa ya chakula awaambie wale*

*walioalikwa, Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa tayari.*

*18 Wakaanza wote kutoa udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, Nimenunua shamba, sharti niende nikalitazame; tafadhali unisamehe.*

*19 Mwingine akasema, Nimenunua ng'ombe jozi tano, ninakwenda kuwajaribu; tafadhali unisamehe.*

*20 Mwingine akasema, Nimeoa mke, na kwa sababu hiyo siwezi kuja.*

*21 Yule mtumwa akaenda, akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi, yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete.*

*22 Mtumwa akasema, Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi.*

*23 Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa.*

> *24 Maana nawaambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu".*

Hivyo na sisi tusitoe udhuru katika mambo ya ki-Mungu, unapoitwa uokoke, hata kama unazo sababu elfu za kutokuacha hicho unachokifanya ikiwa Mungu anataka ukiache, tii tu. Kwasababu hatuwezi kumshawishi Mungu kwa mitazamo yetu tu, kwa vile tuonavyo sisi kuwa ni bora, au vafaa Zaidi kwasasa, naye akashawishika, bali anaelewa kila kitu, na matokeo ya vyote mwishoni utakuwaje..

Hatuna budi, kumtii Mungu.

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:
Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au
Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

UTAYAFIKIAJE MANENO SAFI YA MUNGU?[1]

Utii ni nini? na ni nani tunayepaswa kumtii au kutokumtii?[2]

KUWA MWAMINIFU KWA MANENO YAKO MWENYEWE,[3]

AKETIYE MAHALI PA SIRI PAKE ALIYE JUU.[4]

NI VIZURI SISI KUWAPO HAPA.[5]

VIACHENI VYOTE VIKUE HATA WAKATI WA MAVUNO.[6]

MWENGE WAKO WA UHURU UPO WAPI?[7]

Rudi nyumbani[8]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. UTAYAFIKIAJE MANENO SAFI YA MUNGU?: https://wingulamashahidi.org/2021/09/27/utayafikiaje-maneno-safi-ya-mungu/
2. Utii ni nini? na ni nani tunayepaswa kumtii au kutokumtii?: https://wingulamashahidi.org/2020/01/18/utii-ni-nini-na-ni-nani-tunayepaswa-kumtii-au-kutokumtii/
3. KUWA MWAMINIFU KWA MANENO YAKO MWENYEWE,:

https://wingulamashahidi.org/2020/08/16/kuwa-mwaminifu-kwa-maneno-yako-mwenyewe/

4. AKETIYE MAHALI PA SIRI PAKE ALIYE JUU.: https://wingulamashahidi.org/2022/01/08/aketiye-mahali-pa-siri-pake-aliye-juu/
5. NI VIZURI SISI KUWAPO HAPA.: https://wingulamashahidi.org/2021/02/05/ni-vizuri-sisi-kuwapo-hapa/
6. VIACHENI VYOTE VIKUE HATA WAKATI WA MAVUNO.: https://wingulamashahidi.org/2022/04/27/viacheni-vyote-vikue-hata-wakati-wa-mavuno/
7. MWENGE WAKO WA UHURU UPO WAPI?: https://wingulamashahidi.org/2022/04/02/mwenge-wako-wa-uhuru-upo-wapi/
8. Rudi nyumbani: https://wingulamashahidi.org